# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA – MIKINDANI

## SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MTWARA

**SIMU:** 023-2333299 AU
Makamu 0717115098
Malezi 0787425666
Matron 0713943566
Patron 0712280710
Mtaaluma 0784225245

**Mkuu wa Shule** 0713830862
**Email:***mtwaratech73@gmail.com*

S.L.P. 104,
MTWARA.
Tarehe: 14/11/2025

**Kumb.Na:** MTS/F.I/VOL.III/

**Jina la Mwanafunzi** ........................................................................

**S.L.P.** ………………………………....
…………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MTWARA ILIYOPO WILAYA YA MTWARA-MKOA WA MTWARA MWAKA 2026**

## 1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule hii mwaka **2026.** Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara ipo umbali wa **Km 2** Kaskazini Magharibi mwa mji Mkuu wa Mkoa/ Halmashauri ya **Manispaa ya Mtwara – Mikindani.**

Usafiri wa basi kutoka mjini **Mtwara** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Mtwara (Mkanaledi).** Nauli ni **TShs 2000/= kwa Bodaboda, TShs 3000/= kwa Bajaji na TShs. 5,000/= kwa Tax.**

Muhula wa masomo unaanza Januari **2026.**

Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara ni shule ya Mchepuo wa Amali ya uhandisi, mwanafunzi anasoma somo moja la fani Pamoja na masomo mengine shiriki ya amali.

- **Fani za amali ya uhandisi zinazofundishwa ni:**

i. Carpentry and Joinery with metal work
ii. Electrical installation
iii. Welding and metal fabrication
iv. Plumbing and pipe fitting
v. Masonry and brick laying

- **Masomo mengine shiriki ya amali ni:**

i. Mathematics
ii. English language
iii. Business studies
iv. Historia ya Tanzania na maadili
v. Life skills
vi. Computer application
vii. Engineering science
viii. Technical drawing

## 2.0 Mambo Muhimu ya kuzingatia.

**2.1 Sare ya shule.**

a) Sare ya Shule ni kama ifuatavyo:-

**Wavulana-** MASHATI MEUPE mawili (2) yenye mikono mifupi, SURUALI mbili (2) rangi ya KAKI na zenye malinda mawili au matatu, zenye upana chini 16 -18, VIATU VYEUSI vya kufunga na kamba na SOKSI NYEUPE pea mbili, na MKANDA MWEUSI usio na nembo zozote au picha yoyote.

Pia aje na OVAROLI rangi ya Bluu kwa ajili ya masomo ya ufundi kwa vitendo

**Wasichana**- MASHATI MEUPE mawili yenye mikono mifupi, SKETI mbili RANGI YA KIJANI zilizo ndefu hadi chini (USAWA WA KIFUNDO MGUU) na zenye malinda na UFITO MWEUPE CHINI YA MAGOTI, VIATU VYEUSI vya kufunga kwa kamba na SOKSI NYEUPE pea mbili. Kwa wanaovaa Hijab (NUSU KANZU) , vazi hilo linatakiwa lifanane na Sare za Shule pamoja na nguo za kushindia.

Pia aje na OVAROLI rangi ya Bluu kwa ajili ya masomo ya ufundi kwa vitendo.

**Nguo za kushindia** (Shamba Dress)- Anatakiwa awe na Tshirt mbili (2) rangi ya kijani zenye nembo ya shule ili kuleta mfanano (Hizi zinapatikana shuleni).Suruali moja au mbili rangi ya kahawia (brown) kwa wavulana na Gauni moja au mbili rangi ya kahawia (brown) kwa wasichana.

**NB: Kwakuwa kuna tatizo la Wazazi/Walezi kukosea rangi, malighafi, mtindo na hivyo kupelekea sare na nguo za kushindia kuwa tofauti na zile zinazohitajika shuleni, Mzazi/Mlezi ANASHAURIWA ashonee shuleni.**

**b) Sare ya Michezo**

Wavulana: Tracksuit mbili rangi ya Blue, Bukta mbili rangi ya Blue, Fulana ya michezo rangi ya Blue na Raba za Michezo.

Wasichana: Tracksuit mbili rangi Blue, Fulana ya michezo rangi ya Blue na Raba za Michezo.

**2.2 Vifaa vya kujifunzia**

Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kujifunzia awapo shuleni: Daftari 12 aina ya Counter Book, kalamu na Penseli za kutosha, Mkebe wa Hesabu na rula.

**2.3 Matibabu**

Matibabu ni jukumu la mazazi/mlezi hivyo Mwanafunzi anapokuja shuleni aje na fedha za kutosha atakazotumia kwa ajili ya matibabu pindi akiugua pamoja na fedha ya matumizi yake binafsi (Pocket Money).

NB:ENDAPO MWANAFUNZI HANA BIMA YA AFYA AJE NA Sh 50,400/- KWA AJILI YA KUTENGENEZEWA BIMA YA MWAKA MMOJA YA MFUKO WA BIMA (NHIF).

### 1.1 2.4 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

a) Mzazi utamlipia mwanao nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

b) Mwanafunzi aje na Godoro lenye urefu wa futi 6 na upana futi 2.5 na mto wa kulalia.Ukipenda utanunua shuleni.

NB: **GODORO LIWE NA COVER NGUMU**

c) Mwanafunzi aje na SHUKA jozi mbili (jozi moja rangi ya Pink na jozi ya pili rangi ya Blue)

d) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula

e) Ndoo mbili kwa ajili ya kuogea na kufulia. Ukipenda utanunua shuleni.

f) Chandarua kwa ajili ya kujikinga na Mbu waenezao vimelea vya Malaria.

g) Madaftari (kaunta book) zisizopungua 12

h) **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

i) Nguo za ndani za kutosha;

j) Kwanja 1, jembe 1, mifagio 2 wa ndani 1 na wa nje 1, dawa ya chooni lita 5, Panga1 na sqeezer 1.

## 3.0 Sheria na Kanuni za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni **lazima;**
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
i) Kutunza mali za umma;

### 3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/Kupata Mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kufuga ndevu

l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

m) Kukataa adhabu kwa makusudi.

n) Kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya Mwalimu wa Zamu, Makamu Mkuu wa Shule au Mkuu wa Shule

**o) KUMILIKI, KUKUTWA AU KUTUMIA SIMU YA MKONONI KATIKA MAZINGIRA YA SHULE.**

## 4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi.

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

## 4.1 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza Kikamilifu

**.NB: Tafadhali uje na fomu zilizotajwa kipengele 4.0, usipokuja nazo itaathiri usajili wa kijana wako**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

..................................................

**RIYADH KADHI.**

**MKUU WA SHULE.**

## A. MEDICAL EXAMINATION FORM (HATI YA DAKTARI)

**Mtwara Technical Secondary School,**
**P.O.Box 104,**
**MTWARA.**
**Date................................**

TO THE MEDICAL OFFICER**,**

……………………………….............................,

NAME: …………………………......................................................

Please examine the above named as to his /her fitness for further education at Mtwara Technical Secondary School in the areas;

| | **NORMAL** | **NOT NORMAL** |
|---|---|---|
| EYES | | |
| EARS | | |
| RESPIRATORY SYSTEM | | |
| GIT | | |
| CVS | | |
| URINE/STOOL | | |
| VDRL | | |
| STOMACH ULCERS | | |

...................................

**RIYADH A KADHI.**

**HEADMASTER**

**MEDICAL CERTIFICATE** (To be completed by the Medical Officer)

I have examined the above named consider that he/she is.........................................................

..........................................................................take up the studies.

Date…………………. Name and signature ....……………………............................

Station………………. Designation……………………………

## B. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.

**Historia ya mwanafunzi**

1. Jina la Mwanafunzi............................................................. Jinsia (ME/KE) .................
   Umri................ Tarehe na Mwaka aliozaliwa ................................................
2. Shule ya Msingi aliyosoma awali............................................. Uraia...............................
3. Mahali anapoishi; Kijiji/Mtaa.................................Wilaya....................Mkoa...................
4. Unaishi na Wazazi/Mlezi/Yatima....................... .........................................
5. i) Kama unaishi na Mzazi:
   Jina la Baba/Mama ........................................... Mahali anapoishi ..........................

   ii) Kama unaishi na Mlezi:
   Jina la Mlezi .......................................... Mahali anapoishi .................................

   iii) Kama wewe ni Yatima:
   Jina la anayekuhudumia .................................... Mahusiano ................................

Picha ya mzazi (baba)/Mlezi wa kiume
Jina: .........................................

Picha ya mzazi (mama)/Mlezi wa kike
Jina: ................................................

**Mkataba wa Kutoshiriki katika Migomo, fujo ma makosa ya jinai.**

Mimi ...........…………………………...…niliyechaguliwa kujiunga na Kidato cha .................. mwaka ............... nimesoma na kuyaelewa maelezo ya kujiunga na Shule ya Sekondari ya Ufundi Mtwara na ninaahidi kwamba:-

1. Nitafuata na kutekeleza Sheria na Kanuni zote za Shule hii.
2. Naahidi kutoshiriki katika migomo ya aina yoyote, fujo na makosa ya Jinai.
3. Endapo nitaenda kinyume Sheria na Kanuni zote za Shule hii na kushiriki katika migomo ya aina yoyote, fujo na makosa ya Jinai, **HATUA KALI ZA KINIDHAMU** zichukuliwe dhidi yangu.

Tarehe…………………… Sahihi……………………………..

**C. FOMU YA MZAZI/MLEZI** (Ijazwe na Mzazi/Mlezi Mwenyewe)

Mimi…………………………..............................ambaye ni mzazi/mlezi wa kijana wangu aitwae ………………….................................…nakubaliana na Sheria na Kanuni za Shule. Nitayakubali na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule hii.

Tarehe……………………  Sahihi…………………………

**TAARIFA ZA DHARULA**

Tafadhari orodhesha ndugu ambao shule inaweza kuwasiliana nao wakati wa dharula

| NA. | JINA | MAHALI ANAPOISHI | NAMBA YA SIMU | MAHUSIANO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |

.